

Public education
Discover a world of opportunities

SAYANSI: KUSOMEA NYUMBANI

SAYANSI NYUMBANI

Jifanye kuwa mwanasayansi

Ni rahisi kuwa mwanasayansi – mtoto wako anahitaji vitu vitatu rahisi:

1. Akili iliyotulia: Himiza mtoto wako kuhoji kila kitu karibu yao - hii inawafanya wanasyansi vijana wa ajabu!
2. Kioo cha kuongeza ukubwa: Ruhusu mtoto wako kugundua dunia kwa undani mkubwa sana.
3. Mkoba wa thamani: Ruhusu mtoto wako kukusanya vitu ambavyo vinaweza kuvutia, kwa mfano maganda, mawe madogo, majani na manyoya. Ruhusu nafasi nyumbani kwao ya kuonyeshea hazina zao au kuwaweka katika mifuko maalum na masanduku.

Kuchezea kwenye maji

- Jaribu vitu mbalimbali kwenye maji kuona kama vinaelea au kuzama. Fanya utabiri kabla ya kuwapima. Uliza mtoto wako maswali kama: *Kwa nini baadhi ya vitu vinaelea na vingine vinazama? na Jinsi gani unaweza kufanya kitu kuzama au kitu kinachozama kueleka?*
- Kuuliza mtoto wako kufikiri sehemu ambapo maji yanakotoka na sehemu yanakokwenda yakimwagika.
- Kutumia vyombo vilivyozeeka kupuliza hewa na maji. Bonyeza chombo kitupu kwenye mikono ya mtoto wako na kuwauliza jinsi wanavyojisikia. Jaza chombo kwa maji na kuuliza mtoto wako kubonyeza maji nje. Jaribu kufanya hivi chini ya maji. Fanya majoribio kwa kufanya mwelekeo juu ya ukuta.

Wakati wa usiku

- Tembea usiku kwa kutumia tochi. Fanya kivuli kwenye ukuta. Jenga hadithi kwa kivuli cha kikaragosi.
- Tazama anga wakati wa usiku. Kwenda kwa kutembea katika bustani bila tochi na kuuliza mtoto wako maswali kama: *Unaona nini? Unasikia nini? na Kitu gani kinaweza kufanya kelele hizo?*



Department of
Education

Utajua zaidi

Kijitabu cha ukweli wa kusomea nyumbani
Kwenye education.wa.edu.au.